



FAIDA ZILIZOMO KATIKA KATIBA INAYOPENDEKEZWA KWA WANAWAKE WA KENYA

- ♀ Watoto wataweza kupata uraia wa Kenya kupitia kwa mama zao, hata kama mama zao hawakuolewa na raia wa Kenya. Kifungu cha 14 (1).
- ♀ Watu watakaooana watakuwa na haki sawa wakati wa kufunga ndoa, wakati watakapokuwa wakiishi pamoja kama mke na mume na hata wakati wa kutengana au kuachana. Kifungu cha 45 (3).
- ♀ Katiba inayopendekezwa inahakikisha kuwa jukumu la kuwalea watoto litakuwa juu ya wazazi wote wawili pasipo kujali kama wameoana au la. Kifungu cha 53 (1) (e).
- ♀ Katiba inayopendekezwa inaondoa ubaguzi wa kijinsia katika maswala ya ardhi na mali na inawapa haki sawa wote, wanawake wa wanaume, katika kurithi na kupata ardhi katika Kifungu cha 60 (1) (f).
- ♀ Katiba inayopendekezwa itatoa nafasi ya kuundwa kwa sheria itakayolinda mali ya familia, hasa nyumba ya familia, wakati wa ndoa na hata baada ya kuvunjika kwa ndoa. Kifungu cha 68 (c) (iii).
- ♀ Katiba inayopendekezwa inashikilia kuwa katika kila kundi ambamo kutafanywa uchaguzi, kuwe na angalau theluthi moja ya wanawake au wanaume. Jambo hili linahakikisha kuwa, kwa uchache kabisa, kutakuwa na angalau mwanamke mmoja kwa kila wanaume watatu wanaochaguliwa. Kifungu cha 81 (b).



Katiba inayopendekezwa inahakikisha kwamba kutakuwa na usawa baina ya wanaume na wanawake katika vyama vya kisiasa kwa kusisitiza kuwa vyama vya kisiasa na makundi mengine yanadumisha na kukuza usawa huo wa kijinsia. Kifungu cha 91 (f).



Katiba inayopendekezwa inaeleza kuwa Bunge litatunga sheria ya kuongeza uwakilishaji bungeni wa wanawake, watu wenye ulemavu, makundi ya kijamii na makundi mengine ambayo yamesahaulika au kupuuzwa. Kifungu cha 100.



Wanawake na wanaume watakuwa na haki ya kutunzwa kwa njia sawa na kupata nafasi sawa katika nyanja za siasa, uchumi, utamaduni na jamii, pasipo kubaguliwa. Kifungu cha 27 (3).



Katiba inayopendekezwa inahakikisha haki ya afya nzuri ikiwa ni pamoja na afya ya uzazi kwa wote. Kifungu cha 43 (1) (a).



Kanuni za Tume ya Utumishi wa Umma katika Katiba inayopendekezwa zinatoa nafasi nyingi na zenye usawa wa uteuzi, mafunzo na kujiendeleza baina ya wanaume na wanawake katika viwango vyote vya utumishi wa umma. Kifungu cha 232 (i).



NAIROBI

Federation of Women Lawyers, Kenya (FIDA-K),
Amboseli Road, Off Gitanga Road
P.O Box 46324-00100, Nairobi
Tel: 254 (020) 3870444/3873511/3864030
Fax: 254 (020) 387 637 2
Mobile: 254 (722) 509 760 or 254 (733) 845 003
Email: info@fidakenya.org
www.fidakenya.org

MOMBASA

Federation of Women Lawyers, Kenya (FIDA-K),
Kizingo East Road, next to Lake Side Apartments
Off Mama Ngina Drive
P.O. Box 80687-80100, Mombasa
Tel: 041-2224500/041-2313611
Fax: 041-2224492
Mobile: 0724-256 659/0724-444 449
Email: info@msa.fida.org
www.fidakenya.org

KISUMU

Federation of Women Lawyers, Kenya (FIDA-K),
Milimani Estate, Off Tom Mboya Drive
P.O. Box 19219-40100, Kisumu
Tel: 057 2025560, Tel/Fax: 057 2023160
Mobile: 0724-256658/0734 444 448
Email: info@fidaksm.org
www.fidakenya.org